فَضْلُ الْمَدِيْنَةِ

وَآدَابُ سُكْنَاهَا وَزِيَارَتُهَا

FADHLA ZA MADINA

NA ADABU ZA WAKAAZI WAKE NA WENYE KUTEMBELEA MADINA

إِعْدَاد

عبد المحسن بن حمد العباد البدر

IMEFASIRIWA NA:

ABUU HASHIM ABDULKADIR BIN HASHIM

1431 HIJRA SAWA NA 2010

Yaliyomo

Pongezi na Shukrani II

Fadhla za Madina 2

Fadhla za Msikiti wa Mtume ﷺ 9

Fadhla za Masjid Qubaa 14

Adabu za kuishi Madina 16

Adabu za Kuzuru Madina 22

Fadhla za Abu Bakr na 'Umar (رضي الله عنهما) 24

Ziara za Uzushi 27

Faida Tatu za Mwenye Kuzuru Makaburi 36

Pongezi na Shukrani

Shukrani zote ni za Allah Mtukufu, na Swala na Salamu zimfikie Mtume wetu, na Ahli zake na Maswahaba wake wote.

Kitabu hiki kiitwacho " Fadhlul Madiina wa Aadaabu Suknaahaa wa Ziyaaratuhaa" ni kitabu kinachoelezea Fadhla za Mji wa Madina, na Adabu za kuishi humo na ziara za kisheria zilizomo humo.

Ni kitabu kilichoandikwa na Mwanachuoni Mkubwa katika Mji wa Madina, Assheikh Abdul Muhsin Bin Hamad Al Abbaad Al Badru Allah Amhifadhi.

Kutokana na faida kubwa na za kipekee zilizomo kwenye kitabu hiki: Ni jambo jema sana kufasiriwa kwenye lugha yetu ya Kiswahili, ili wasioijua lugha ya kiarabu waweze kupata faida hizo.

Shukran kubwa pamoja na Pongezi zetu zimuendee Shekhe Mbora, Abuu Haashim Abdul Qaadir Bin Haashim Allah Amhifadhi, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kukifasiri kitabu hiki kwenye lugha yetu ya Kiswahil, Allah Amlipe Kheri.

Mwanachuoni mwingine wa Madina Assheikh Aburrazzaaq Allah Amhifadhi, ambaye ni Mtoto wa Shekhe Abdul Muhsin Bin Hamad Al A'bbaad Al Badru: alinipa jukumu la kuipitia tafsiri hiyo " tarjama", na nilifanya hivyo mwanzo mpaka mwisho, ambapo sikuona makosa yoyote makubwa ya kiitikadi kwenye tafsiri, na yale madogo madogo machache ya kiuandishi niliweza kuyasahihisha.

Tunataraji kwa kufasiriwa kitabu hiki kwenye kiswahili: kutatoa msaada mkubwa sana kwa Waislamu wanaouzuru mji wa Madina kwenye misimu ya Hija na Umra, wa kuzijua Adabu za kuishi kwenye mji huu, pamoja na ziara zake za kisheria, na Fadhla za kuswali kwenye Msikiti wa Mtume Swalla Llaahu Alaihi Wasallam..

Imeandikwa na:
Khamis Imam Hussein.
Mwanafunzi chuo kikuu cha Kiislamu cha Madina-Saud Arabia.
Kitengo cha D'awa na Utamaduni wa Kiislam.
Kiwango cha (PHD)

14/ Ramadhan/ 1438 H
9/ Jun/ 2017 M

Utangulizi

Sifa njema zinamstahiki Allaah (عز وجلّ), na rehema na amani zimshukie Mtume Wetu Muhammad ﷺ, na jamaa zake, na maswahaba wake wote.

Kitabu hiki kidogo kilichotungwa na mwana wa chuoni Sheikh ‘Abdul-Muhsin Al-‘Abbaad Al-Badr; ni kitabu chenye faida nyingi ambazo huwezi kuzipata katika vitabu vingi.

Na sababu za kufasiri kitabu hiki ni:

1. Madina Ni mji wa Mtume Rehma na amani zimshukie.
2. Kuwepo kwa msikiti mtukufu wa pili baada ya Masjid-il-Haraam wa Makkah.
3. Ili watu wajue kuwa yale mambo yaliyoharamishwa kufanywa Makkah, pia ni haraam kuyafanya Madinah.
4. Watu wengi wanadhani kuwa mji mtukufu ni Makkah peke yake ndiyo nikafasiri ili watu hao wajue kuwa mji huu wa Madinah pia ni mtukufu.
5. Mimi naupenda mji huu wa Madinah.

Na ninamuomba Allaah aijaalie amali hii iwe na ikhlaas. Pia ninamuomba Allaah anisamehe madhambi yangu, na ya wazazi wangu, na ya waislamu wote.

ABU-HASHIM ABDULKADIR HASHIM,
13/9/1431,
23/8/2010.

Ama baad, hakika mji wa Mtume Mtukufu ﷺ Twayibat Twayyiba ndiyo mashukio ya waha'i , na ndipo aliposhuka Jibril mwaminifu kwa Mtume Mtukufu ﷺ, na nishina. ndio marejeo ya imani na ndio makutano ya muhajirina na Answar na ndio mahali pa wale ambao wamechagua mji na Imani, na Madina ndio mji mkuu wa Kwanza wa waislamu, huko ndiko kulikofungwa bendera za Jihadi katika njia ya Allaah, vikaenda vikosi vya haki katika kuwatoa watu katika giza kuwatia katika mwangaza, na huko ndiko kulikoenea mwangaza, ardhi ikanawiri kwa mwangaza wa hidaya, na Madina ndio mji aliohamia Mtume ﷺ alihamia hapo na akaishi hapo mpaka mwisho wa uhai wake ﷺ na alikufa hapo, na alizikwa hapo, na atafufuliwa kutoka hapo Madina, na kaburi lake ndilo kaburi la kwanza litakalopasuka (nayeye ndie wakwanza atakayefufuliwa) na hakuna uhakika wa mahali palipo na kaburi lolote katika Mitume ispokuwa mahali pa kaburi lake Mtume ﷺ

Na mji huu wenye kubarikiwa, Allaah ameutukuza na kuujalia ndio mahali bora baada ya makkah, na dalili ya kufahamisha ubora wa Makkah kuliko Madina ni neno la Mtume ﷺ wakati makafiri walipomtoa Makkah na akaelekea Madina hali ya kuhamia, akasema Mtume ﷺ kwa kuuambia mji wa Makkah:

« وَاللّهِ إِنّكِ لَخَيْرُ أَرْضِ اللّهِ وَأَحَبُّ أَرْضِ اللّهِ إِلَى اللّهِ وَلَوْلاَ أَنِّى أُخْرِجْتُ مِنْكِ مَا خَرَجْتُ »

Na-aapa kwa Allaah hakika yawewe ni bora ya ardhi ya Allaah na umpendwa zaidi wa Allaah kuliko ardhi nyengine ya Allaah na lau mimi nisingetolewa kwako nisingetoka". [Amepokea Tirmidhi na ibn Majah nayo ni hadeeth swaheeh].

ama hadeeth inayonasibishwa na Mtume ﷺ kuwa aliomba na kusema: "*Ewe Mola wangu wa haki hakika Wewe umenitoa katika mji ninao upenda zaidi kuliko miji yote*" – anakusudia Makkah ni jaalie katika mji unaoupenda zaidi kuliko miji yote –anakusudia Madina" (Hiyo ni hadeeth maudhui) na maana yake haipo sawa; kwani hadeeth hiyo inafahamisha kuwa: mji anaoupenda zaidi Allaah sio anaoupenda zaidi mtume ﷺ na mji anaoupenda zaidi Mtume sio anaoupenda Allaah, na katika mambo yanayojulikana nikuwa: mapenzi ya Mtume ﷺ ni yenye kufuata mapenzi ya Allaah (سبحانه وتعالى) Haliwezi kuwa alipendalo Allaah silo alipendalo Mtume ﷺ.

Nimeonelea niandike risala hii inayoelezea fadhla za mji huu wenye kubarikiwa na kuweka wazi adabu za kuishi katika mji huo na kuzuru katika mji huo, kwa hiyo nitataja jumla ya fadhla zake kisha jumla katika adabu za kuishi huko Madina kisha jumla katika adabu za kuzuru mji huo:

na katika fadhila za mji huo wenye kubarikiwa ni kuwa:
Allaah (سبحانه وتعالى) ameujaalia mji huo kuwa Mtukufu wenye amani kama alivyoujaalia Makkah kuwa ni mji Mtukufu wenye amani, na imekuja kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema:

« إِنّ إِبْرَاهِيمَ حَرّمَ مَكّةَ وإِني حَرّمْتُ الْمَدِينَةَ »

"*Hakika Ibrahim ameufanya Makkah kuwa ni mji Mtukufu na mimi nimeifanya Madina kuwa ni mji Mtukufu*". [Ameipokea hadeeth hiyo Muslim].

Na makusudio ya kufanya utukufu kuliko nasibishwa na mtume ﷺ na Ibrahim (عليه السلام) ni kudhihirisha huo utukufu kwani huko kutukuza kumefanywa na Allaah, nae ndiye aliyeufanya mji wa makka kuwa mtukufu na akaufanya huu wa madina kuwa mtukufu). Na Allaah (عز وجل) amekhusisha miji hii miwili kwa sifa hiyo ya utukufu kuliko miji mengine iliyobaki. na haikuja dalili yoyote iliyothibiti inayofahamisha utukufu wa kitu chochote isipokua Makkah na Madina. Na yaliyoenea katika ndimi za watu wengi kuwa Al-masjidul Aqswa ndiyo haramu ya tatu; hilo ni katika makosa yalioenea. kwani hakuna haram ya tatu, lakini msemo ulio swaheeh ni kusema Masjidul Aqswa ni msikiti wa tatu katika misikiti miwili iliyotukuzwa, na imekuja hadeeth kutoka kwa Mtume ﷺ inayofahamisha fadhla za misikiti hii mitatu na fadhla za kuikusudia kwa ajili ya kuswali humo, wakati Mtume ﷺ: aliposema:

« لاَ تُشَدُّ الرِّحَالُ إِلاّ إِلَى ثَلاَثَةِ مَسَاجِدَ مَسْجِدِ الْحَرَامِ ومسجدي هَذَا ومَسْجِدِ الأَقْصَى »

"*Haifungwi misafara isipokuwa kwa ajili ya misikiti mitatu Al-Masjidul haram na msikiti wangu huu na msikiti wa Aqswaa.*" [Bukhary na Muslim].

Kisha makusudio ya Haram katika Makkah na Madina: ni sehemu inayozungukwa na mipaka katika kila moja ya hiyo miji miwili; hiyo ndiyo haram, na jina lililoenea la kuita haram[sehemu tukufu] msikiti wa Mtume peke yake; hilo ni katika makosa yenye kuenea. kwani si msikiti peke yake ndio sehemu tukufu bali mji wote ni mtukufu. Sehemu iliyo baina ya Jabal Air na Thaur na sehemu iliyomo baina ya mitaa yake miwili. na amesema Mtume ﷺ:

« الْمَدِينَةُ حَرَمٌ مَا بَيْنَ عَيْرٍ إِلَى ثَوْرٍ »

"*Madina ni mji mtukufu; sehemu iliyo baina ya Jabal 'Air mpaka Thaur*" [Ameipokea Bukhary na Muslim].

Na amesema Mtume ﷺ:

« إني أُحَرِّمُ مَا بَيْنَ لاَبَتَيِ الْمَدِينَةِ أَنْ يُقْطَعَ عِضَاهُهَا أَوْ يُقْتَلَ صَيْدُهَا »

"*Mimi nimeharamisha sehemu iliyo baina ya mitaa miwili ya Madina; kukatwa miti yake au kuuwawa kiwindwa chake*". [Ameipokea hadeeth hiyo Muslim]

Na katika mambo yanayojulikana nikuwa: Madina imepanuka kwa sasa; mpaka sehemu nyengine zimetoka nje ya haram[sehemu tukufu], kwa hivyo haisemwi kuwa majumba yote yalioko Madina ndio haram. ila nyumba zilizokuwa ndani ya mipaka ya haram ndio haram, na zilizokuwa nje ya mipaka ya haram zinaitwa kuwa ziko Madina na haisemwi kuwa ziko haram. Na imekuja hadeeth kutoka kwa Mtume Mtukufu ﷺ katika kuweka wazi mipaka ya haram ya Madina kuwa: haram ni sehemu iliyo baina ya mitaa miwili au iliyo baina ya majabali mawili : Jabal Air mpaka Jabal Thaur. na haya matamko mawili hayapingani; kwani lafdhi ndogo inaingia katika lafdhi kubwa, kwa hiyo sehemu iliyo baina ya mitaa miwili ni haram na baina ya Jabal 'Air mpaka Thaur ni haram, na likitatiza jambo katika sehemu yoyote inawezekana kuwa ni katika haram na inawezekana kuwa si katika haram, kwani hii inafanana zaidi na yanayosemwa kuwa ni katika mambo yenye kutatiza. na mambo yenye kutatiza: Mtume ﷺ amebainisha njia inayofuatwa katika mambo hayo. na njia yenyewe ni kujitoa katika shaka (ihtiyat) kama alivyosema Mtume ﷺ katika hadeeth ya Nu'man Ibn Bashir (رضي الله عنه), hadeeth iliyoafikiwa uswaheeh wake:

« فَمَنِ اتّقَى الشُّبُهَاتِ فقد استبرأ لِدِينِهِ وَعِرْضِهِ، وَمَنْ وَقَعَ فِي الشُّبُهَاتِ وَقَعَ فِي الْحَرَامِ »

"Mwenye kujiepusha na mambo yenye kutatiza atakuwa ameitakasa dini yake na heshima yake. na mwenye kuingia katika mambo yenye kutatiza ameingia katika haramu."

na katika fadhla ambazo zimekuja katika swala zima la mji huu wa Madina wenye kubarikiwa ni kuwa: Mtume ﷺ ameuita: Twaiba na Twaaba. na imethibiti katika swaheeh Muslim kuwa : Allaah ameuita Mji huu Twaaba. Mtume ﷺ amesema:

« إِنّ اللّهَ تَعَالَى سَمّى الْمَدِينَةَ طَابَةَ »

"hakika Allaah ameuita mji wa Madina Twaba"

Na matamshi haya mawili yamechukuliwa kutokana na Twayyib na yafahamisha kitu kizuri. kwa hivyo hayo ni matamshi mawili mazuri yameitwa ardhi nzuri.

Na katika fadhla za Mahina ni kuwa: imani inarejea Madina. kama alivyosema Mtume ﷺ:

« إِنّ الإِيمَانَ لَيَأْرِزُ إِلَى الْمَدِينَةِ كَمَا تَأْرِزُ الْحَيّةُ إِلَى جُحْرِهَا »

"Hakika imani inarejea Madina kama nyoka anavyorejea katika tundu lake" [Amepokea Bukhari na Muslim)".

Na maana yake ni kwamba: imani inaelekea Madina na inapatikana huko Madina na waislamu wanaikusudia Madina. imani inawapelekea hilo na kuipenda ardhi hii yenye kubarikiwa. na Allaah ameitukuza.

Na katika fadhla zake : ni hadeeth iliyokuja kutoka kwa Mtume ﷺ ambayo ameisifu Madina kuwa: ni kijiji kinachokula vijiji vyengine. Mtume ﷺ: amesema:

« أُمِرْتُ بِقَرْيَةٍ تَأْكُلُ الْقُرَى... »

"Nimeamrishwa kuhamia katika kijiji kinachokula vijiji vyengine."

ana kusudia kuwa ameamrishwa kuhamia katika kijiji hicho kinacho kula vijiji vyengine.

« يَقُولُونَ يَثْرِبُ ، وَهِي الْمَدِينَةُ »

"Wanauita huo mji Yathrib nao ni Madina" [Amepokea Bukhari na Muslim]

na neno la Mtume ﷺ "تَأْكُلُ الْقُرَى"linafasiriwa kuwa: ni mji unaonusurika na utakaopata ushindi kuliko vijiji vyengine, na imefasiriwa kuwa ni mji unaoletewa ghanima zinazopatikana katika vita vya Jihadi katika njia ya Allaah. na kila moja katika mambo haya mawili yametokea na kupatikana: kumepatikana kushinda kwa mji huu kuliko miji mingine, kwani walitoka watu waongofu wenye kusuluhisha na wanajeshi wenye kufungua miji na wakawatoa watu katika giza na kuwatia katika mwangaza kwa idhini ya Mola wao, na wakaingia watu katika dini ya Allaah Mtukufu, na kila kheri iliyopatikana kwa watu ilitokea katika mji huo wa Madina uliobarikiwa, mji wa bwana Mtume ﷺ.

na kuwa mji huu unanusurika kuliko vijiji vyengine: yaani kunusurika kwake kuliko miji mingine; kama ilivyotokea katika zama za kwanza pamoja na mashujaa wa kwanza; maswahaba wa bwana Mtume ﷺ, na Makhalifa waongofu; Allaah awaridhie. na vile vile kupatikana ghanima na kuzipeleka

Madina: hili pia lilipatikana. kwani Mtume ﷺ alielezea kuzitoa mali za Kisra na Kaisar katika njia ya Allaah Mtukufu, na hili lilipatikana. zililetwa Mali hizo katika mji wa Madina wenye kubarikiwa na zikagawanywa kupitia mkono wa Alfaruk Allaah amridhie.

Na katika fadhila za Madina ni kuwa: Mtume ﷺ Alihimiza kusubiri juu ya shida zake na dhiki zake na akasema:

« الْمَدِينَةُ خَيْرٌ لَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ »

"Madina ni bora kwao lau wangekuwa wanajua"

alisema maneno hayo kwa wale waliofikiria kuhama Madina kwenda kwenye sehemu ambazo zina raha na maisha mazuri na mali nyingi. kwasababu hiyo Mtume ﷺ akasema:

« الْمَدِينَةُ خَيْرٌ لَهُمْ لَوْ كَانُوا يَعْلَمُونَ لاَ يَدَعُهَا أَحَدٌ رَغْبَةً عَنْهَا إِلاّ أَبْدَلَ اللّهُ فِيهَا مَنْ هُوَ خَيْرٌ مِنْهُ وَلاَ يَثْبُتُ أَحَدٌ عَلَى لأْوَائِهَا وَجَهْدِهَا إِلاّ كُنْتُ لَهُ شَفِيعًا أَوْ شَهِيدًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ »

"*Madina ni bora kwao lau wangekuwa wanajua" haiachi mtu yoyote kwa sababu ya kuichukia isipokuwa Allaah humbadilishia mtu ambaye ni bora kuliko yeye, na mtu yeyote hatovumilia shida zake na dhiki zake isipokuwa nitakuwa ni mwenye kumwombea shufaa au ni shahidi wake siku ya kiyama*." [amepokea hadeeth hiyo Muslim]

Na hii inatufahamisha fadhla za mji huu na fadhla za kusubiri shida na tabu. na dhiki zikimpata mtu yeyote isiwe ni sababu ya kumfanya mtu ahame kutoka Madina kwenda mji mwengine kwa kutafuta raha na maisha mazuri, bali anatakiwa asubiri kwa lolote linalompata hapo Madina. na ameahidiwa malipo makubwa na thawabu nyingi kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى).

Na katika fadhla za Madina ; nikuwa: Mtume ﷺ ameweka wazi ukubwa wa jambo lake na hatari ya kuzusha mambo hapo Madina wakati alipobainisha utukufu wake, akasema:

« الْمَدِينَةُ حَرَمٌ مَا بَيْنَ عَيْرٍ إِلَى ثَوْرٍ مَنْ أَحْدَثَ فِيهَا حَدَثًا أَوْ آوَى مُحْدِثًا فَعَلَيْهِ لَعْنَةُ اللّهِ وَالْمَلاَئِكَةِ وَالنّاسِ أَجْمَعِينَ لاَ يَقْبَلُ اللّهُ مِنْهُ صَرْفًا وَلاَ عَدْلاً»

"Madina ni Haram (tukufu) sehemu iliyo baina ya jabal 'Air mpaka jabal Thauri, mwenye kuzusha jambo hapo Madina au akamuhifadhi mzushi basi imshukie la'na ya Allaah na malaika na watu wote. Allaah hamkubalii ibada ya faradhi wala ya sunnah."

[Amepokea Bukhari na Muslim)

Na katika fadhla za Madina: ni dua ya kuiombea baraka iliyokuja kutoka kwa Mtume ﷺ . amesema Mtume ﷺ:

« اللّهُمّ بَارِكْ لَنَا فِي ثَمَرِنَا وَبَارِكْ لَنَا فِي مَدِينَتِنَا وَبَارِكْ لَنَا فِي صَاعِنَا وَبَارِكْ لَنَا فِي مُدّنَا »

"Ewe Mola wangu wa haki tubarikie katika matunda yetu na tubarikie katika Madina yetu, na tubarikie katika pishi yetu na tubarikie katika kibaba chetu."

[Amepokea Imam Muslim]

Na katika fadhla za Madina ni kuwa: haiingii Twa'oon wala haingii Dajjal.

Mtume ﷺ: amesema:

« عَلَى أَنْقَابِ الْمَدِينَةِ مَلاَئِكَةٌ ، لاَ يَدْخُلُهَا الطّاعُونُ وَلاَ الدّجّالُ »

"Katika njia za Madina kuna malaika, haingii twaun wala Dajjaal"

[Ameipokea Bukhari na Muslim)

Na kuna hadeeth nyingi sana zinazoelezea fadhla za Madina. na haya niliyotaja ni sehemu tu katika hadeeth hizo zilizo katika Bukhari na Muslim au katika moja yao. Na miongoni mwa vitabu vizuri mno vilivyotungwa kuelezea fadhila za Madina; ni kitabu ambacho amekitaarisha sheikh Doktur Swaleh, ibn Hamid Ar-Rifai kwa ajili ya kupata Daraja (ya PHD) katika chuo kikuu cha kiislamu cha Madina (Jamiatil Islamia bil Madina) kwa anwani: "Hadeeth zilizokuja kuelezea fadhila za Madina - Kuzikusanya na kuzisoma" na nawausia wenye kutafuta elimu kurejea kwenye kitabu hicho na kupata faida,

katika mambo ambayo mji huo umekusanya: ni msikiti wa Mtume Mtukufu ﷺ na msikiti wa Qubaa.

Ama msikiti wa Mtume Mtukufu ﷺ; zimekuja hadeeth nyingi kuelezea fadhla zake. katika hizo: ni maneno ya Mtume ﷺ aliposema:

« لاَ تُشَدُّ الرِّحَالُ إِلاّ إِلَى ثَلاَثَةِ مَسَاجِدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ، وَمَسْجِدِي هَذَا ، وَمَسْجِدِ الأَقْصَى »

"Haifungwi misafara isipokuwa kwenda kwenya misikiti mitatu Masjidul Haram na msikiti wangu huu na masjidul Aqswaa" [wamepokea Bukhari ma Muslim].

Kwa hiyo katika mji huu kuna mmoja miongoni mwa hiyo misikiti mitatu iliyojengwa na Mitume, na hiyo ndiyo miskiti ambayo haifungwi misafara ispokwa kwenda misikiti hiyo. na pia imekuja hadeeth inayofahamisha fadhla za kuswali katika msikiti huo, na kwamba swala hapo ni bora kuliko swala alfu moja. amesema Mtume ﷺ:

« صَلاَةٌ في مسجدي هَذَا أَفْضَلُ مِنْ أَلْفِ صَلاَةٍ فِيمَا سِوَاهُ إِلاّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ »

"Swala moja katika msikiti wangu huu ni bora kuliko swala elfu moja katika misikiti mingine isipokuwa katika masjidul Haraam." ["Ameipokea Bukhari na muslim].

Hizi ni fadhla kubwa, na ni msimu katika misimu ya akhera, faida ndani yake ni zenye kuongezwa si kwa mara kumi wala mara mia, bali zaidi ya elfu moja. Na katika mambo yanayojulikana nikuwa: wafanya biashara za kilimwengu wanapo jua kwamba bidhaa zao zinatoka mahali fulani katika wakati flani, basi huwa wanajiandaa kwa msimu huo japo kuwa faida ni nusu au zaidi. lakini faida huko akhera si zaidi ya mara kumi wala zaidi ya mara mia wala mia tano wala mia sita, bali ni zaidi ya elfu?

NA KATIKA MAMBO AMBAYO TUNAZINDUSHWA KUHUSU MSIKITI HUU WENYE KUBARIKIWA NI :

LA KWANZA: kuzidishwa thawabu za kuswali katika msikiti huo kwa zaidi ya alfu moja; hakukufungwa kwa swala ya faradhi bila ya swala ya Sunnah, bali ni zote mbili pamoja. kwani Qauli ya Mtume ﷺ imeachilia kwa kusema (Swala), kwa hiyo faradhi moja ni kwa faradhi elfu moja na Sunnah moja ni kwa Sunnah elfu moja.

LA PILI: kuzidiswa huko kulikokuja katika hadeeth hakuhusiki na sehemu maalum ambayo ndiyo iliyokuwa msikiti katika zama za Mtume ﷺ; bali ni ya sehemu hiyo na kila sehemu iliyonasibishiwa msikiti huo katika zile sehemu zilizozidishwa, na ushahidi wa hayo ni kwamba: makhalifa wawili waongofu, 'Umar na Uthman (رضي الله عنهما), walizidisha msikti huo kwa upande wa mbele. na inajulikana kuwa: imamu na swafu zinazomfuata katika sehemu zilizo zidishwa; ni nje ya msikiti uliokuwa katika zama za Mtume ﷺ. Lau kama sehemu iliyozidishwa haina hukumu ya kile kilichozidishwa, hawa makhalifa wawili wasingezidisha msikiti huo kwa upande wa mbele. na maswahaba

wengi walikuwapo, na hakuna yeyote aliyepinga kitendo cha makhalifa hao. na hilo linafahamisha wazi kuwa kuzidishwa thawabu hakuhusiki na zile sehemu zilizokuwa msikiti wa zama za Mtume ﷺ pekee.

LA TATU: katika msikiti huo kuna sehemu aliyoisifu mtume ﷺ kuwa ni bustani katika mabustani ya peponi. Aliposema katika hadithi yake:

« مَا بَيْنَ بيتي ومنبري رَوْضَةٌ مِنْ رِيَاضِ الْجَنّةِ »

"*Sehemu iliyo baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani katika bustani za peponi*" [Amepokea Bukhari na Muslim]

Na kuihusisha sehemu hiyo kwa sifa hii kuliko sehemu nyengine za msikiti; hufahamisha fadhla zake na kuwa na sifa hiyo pekee. na hilo linakuwa kwa kutekeleza swala za sunnah katika sehemu hiyo, na vile vile kumtaja Allaah na kusoma Qur'ani katika mahali hapo; isipopatikana kumuudhi mtu yoyote katika sehemu hiyo au katika kupafikia . ama swala ya faradhi; kuitekeleza katika swafu za mbele ni bora zaidi, kwa maneno ya Mtume ﷺ aliposema :

« خَيْرُ صُفُوفِ الرِّجَالِ أَوَّلُهَا وَشَرُّهَا آخِرُهَا »

"*Bora ya swafu za wanaume ni swafu ya kwanza na shari ya swafu za wanaume ni swafu ya mwisho*." [Ameipokea Muslim]

Na maneno yake Mtume ﷺ:

« لَوْ يَعْلَمُ النّاسُ مَا في النِّدَاءِ وَالصّفِّ الأَوّلِ ، ثُمّ لَمْ يَجِدُوا إِلاّ أَنْ يَسْتَهِمُوا عَلَيْهِ لاَسْتَهَمُواعَلَيهِ »

"*Lau watu wangejua thawabu zilizoko katika adhana na swafu ya kwanza kisha wasipate nafasi isipokuwa kwa kupiga kura, wangepiga kura kwa ajili ya kupata swafu ya kwanza*" [Ameipokea Bukhari na Muslim].

LA NNE: Msikiti wa Mtume ukijaa waswaliji, mwenye kuja kuchelewa analazimika kuswali barabarani kwa kufuata swala ya Imamu katika pande tatu; (sio kwa upande wa mbele), na anapata thawabu za swala ya jamaa, ama kuzidishiwa thawabu kwa zaidi ya elfu moja; hilo limekhusu mtu ambaye swala yake ilikuwa ndani ya msikiti. kwa maneno ya Mtume ﷺ aliposema: "Swala moja katika msikiti wangu huu ni bora kuliko swala alfu katika misikiti mingine isipokuwa Msjidul Haram." Na mwenye kuswali barabarani hawi ni mwenye kuswali ndani ya msikiti wake. kwa hivyo haitapatikana ziada hiyo ya thawabu.

LA TANO: Imeenea kwa watu wengi kwamba anaefika Madina anawajibika kuswali swala arubaini katika Msikiti wa Mtume ﷺ, kwa hadeeth iliyomo katika Musnad wa Imam Ahmad iliyopokewa na Anas (رضي الله عنه) kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: "Mwenye kuswali swala arubaini katika msikiti wangu na isimkose swala yoyote, huandikiwa kuepukana na moto na kuokoka na adhabu na huepukana na unafiki." Na hiyo ni hadeeth dhaifu haiwezi ikasimamisha hoja. bali jambo lenyewe katika suala hilo ni pana, na anaefika Madina halazimishwi swala maalum katika msikiti wa Mtume ﷺ, bali kila swala katika msikiti hua ni bora kuliko swala alfu bila kuwekwa mpaka au kufungwa kwa swala maalum.

LA SITA: Waislamu wengi wametahiniwa katika miji mingi ya kiislamu kwa kujenga misikiti juu ya makaburi au kuwazika waliokufa katika misikiti. na huenda wakatoa hoja baadhi ya wanaolijulisha hilo; kwa kuwepo kaburi la Mtume ﷺ katika msikiti wake. na utata huo hujibiwa kwamba: Mtume ﷺ ndie aliyejenga msikiti huo mara tu alipofika Madina, na akajenga nyumba zake wanazokaa mama wa waumini karibu na msikiti wake, na katika nyumba

hizo nyumba ya bibi 'Aaisha ndiyo ambayo Mtume ﷺ alizikwa ndani yake, na zikabakia nyumba hizo kama zilivyo nje ya msikiti katika zama za makhalifa waongofu (رضي الله عنهم) na zama za Mu'aawiyah na zama za makhalifa wengine baada yake. na katikati ya ukhalifa wa Bani Umayyah msikiti huo ulipanuliwa, na nyumba ya bibi 'Aaisha ambayo Mtume ﷺ alizikwa ndani yake ikaingizwa ndani ya msikiti, na zimekuja kutoka kwa Mtume ﷺ hadeeth nyingi muhkama (zisizokubali kufutwa) zinazofahamisha uharamu wa kuyafanya makaburi kuwa ni misikiti. katika hadeeth hizo ni hadeeth ya Jundub ibn 'Abdillaah al-Bajaly aliyoisikia kutoka kwa Mtume ﷺ kabla ya kufa kwake kwa misiku mitano, akasema katika hadeeth hiyo: nimemsikia Mtume ﷺ kabla ya kufa kwa siku tano akisema:

« إني أَبْرَأُ إِلَى اللّهِ أَنْ يَكُونَ لي مِنْكُمْ خَلِيلٌ فَإِنّ اللّهَ اتخذني خَلِيلاً كَمَا اتّخَذَ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلاً وَلَوْ كُنْتُ مُتّخِذًا مِنْ أمتي خَلِيلاً لاَتّخَذْتُ أَبَا بَكْرٍ خَلِيلاً أَلاَ وَإِنّ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ كَانُوا يَتّخِذُونَ قُبُورَ أَنْبِيَائِهِمْ وَصَالِحِيهِمْ مَسَاجِدَ أَلاَ فَلاَ تَتّخِذُوا الْقُبُورَ مَسَاجِدَ فإني أَنْهَاكُمْ عَنْ ذَلِكَ »

"Hakika mimi najitakasa kwa Allaah kuwa nina rafiki mwandani katika nyinyi kwani Allaah amenifanya mimi ni rafiki mwandani kama alivyomfanya Ibrahim ni rafiki mwandani na lau ningekuwa ni mwenye kufanya urafiki katika umati wangu ningemfanya Abubakar kuwa ni rafiki, zindukeni! Na hakika watu waliyo kuwa kabla yenu walikuwa wakiyafanya makaburi ya Mitume wao na watu wema wao kuwa ni Misikiti, Zindukeni msifanye makaburi kuwa misikiti kwani mimi nakukatazeni jambo hilo."

[Amepokea Muslim katika swaheeh yake].

Bali mauti yalipomshukia Mtume(صلى الله عليه وسلم) alitahadharisha kufanya makaburi kuwa Misikiti. kama ilivyo katika sahihi mbili kutoka kwa Bibi 'Aaisha na Ibn Abbass (رضي الله عنهما) wamesema: "Yalipomshukia mauti, Mtume ﷺ alikuwa akijifunika nguo katika uso wake, akizinduka huiondoa na husema Allaah awalani Mayahudi na Manaswara wanayofanya makaburi ya Mitume wao kuwa misikiti." Anatahadharisha mambo walioyafanya.
Hadeeth hizi kutoka kwa 'Aaisha na Ibn Abbass na Jundub (رضي الله عنهم) ni muhkama. hazikubali kufutwa kwa hali yoyote, kwani hadeeth ya Jundub ilikuwa ni katika siku zake za mwisho, na hadeeth mbili za 'Aaisha na Ibn Abbass zilikuwa katika wakati wake wa mwisho ﷺ. kwa hiyo haifai kwa Muislamu yoyote kuwacha kufwata hadeeth hizi swaheeh muhkama na kutegemea kitendo kilichopatikana katikati ya zama za bani Umayyah, na kitendo chenyewe ni kuingizwa kaburi katika msikiti wake ﷺ, halafu mtu akatolea dalili kufaa kujenga msikiti juu ya makaburi au kuwazika waliokufa katika misikiti.

Ama Masjid Qubaa: Ni msikiti wa pili katika misikiti miwili iliyo na fadhla kubwa hapa Madina. Na misikiti hiyo miwili imeasisiwa kwa ucha mungu tangu siku ya Kwanza. na imekuja dalili kutoka kwa Mtume ﷺ kwa vitendo vyake na maneno yake inayofahamisha fadhla za kuswali katika msikiti wa Qubaa.

Ama vitendo vyake: imepokewa kutoka kwa Abdillah Ibn Omar (رضي الله عنه) amesema:

« كَانَ النبي - صلى الله عليه وسلم – يأتي مسجد قُبَاءً كل سبت مَاشِيًا وَرَاكِبًا فَيُصَلِّى فِيهِ رَكْعَتَيْنِ »

"Alikuwa Mtume ﷺ akija katika msikiti wa Qubaa kila Jumamosi na alikuwa akija kwa miguu na wakati mwengine akiwa kwenye kipando kisha huswali ndani yake rakaa' mbili." [Amepokea Bukhari na Muslim]

Na ama maneno yake, imethibiti kutoka kwa Sahl Ibn Hunaif (رضي الله عنه): amesema mtume ﷺ:

« مَنْ تَطَهَّرَ في بَيْتِهِ ثُمَّ أَتَى مَسْجِدَ قُبَاءٍ فَصَلّى فِيهِ صَلاَةً كَانَ لَهُ أَجْرِ عُمْرَةٍ »

"Mwenye kujitwaharisha nyumbani kwake kisha akaja Masjid Qubaa akaswali ndani yake Swala; humpatikania thawabu za 'Umrah." [amepokea Ibn Majah na wengine]

Na maneno katika hadeeth hii yasemayo "akaswali ndani yake swala" hukusanya swala ya faradhi na swala ya Sunnah, na haikuja katika Sunnah hadeeth yoyote inayofahamisha fadhila za misikiti mingine iliyoko Madina isipokua misikiti hii miwili tu.

adabu zinazohusiana na ukaaji wa Madina:

hakika mtu ambaye Allaah amemuafikisha kuishi katika mji huu wenye kubarikiwa (Twaybatu at-Twayyibah) anawajibika kuhisi kuwa amepata neema kubwa. kwa hiyo anatakiwa amshukuru Allaah kwa neema hii na amsifu kwa ihsani hii. na pia anawajibika kuhisi yakwamba wengi katika wakaazi wa nchi mbalimbali wanakuwa na shauku kubwa ya kufika Makkah na Madina na kubakia katika miji hii japokuwa kwa muda mchache. na kuna watu wanao kusanya pesa kidogo kidogo kwa miaka mingi ili wapate lengo hili la kufika katika mji wa Madina. na nakumbuka kwamba mmoja wa ma-'Ulamaa wa India alitaja kwamba: mahujaji wakihindi katika siku za nyuma walikuwa wakija kwa majahazi na wanakaa baharini muda mrefu katika safari yao ya kuja Makkah na Madina. na kwamba kuna kundi la watu waliokuwa katika jahazi walipoona nchi kavu ambayo ni Makkah na Madina walimsujudia Allaah kwa kumshukuru wakiwa ndani ya jahazi.

Na kuna adabu nyingi kwa wenye kuishi Madina

Ya Kwanza: muislamu anatakiwa aupende mji huu kwa fadhila zake, na kwa sababu ya Mtume ﷺ kuupenda. Amepokea Bukhari katika swaheeh yake kutoka kwa Anas (رضي الله عنه) kwamba: Mtume ﷺ alikuwa akirudi kutoka safarini akiona kuta za Madina, humuharakisha mnyama wake na akiwa katika kipando hukiharakisha kwa sababu ya kuipenda Madina.

Ya Pili: muislamu akiwa katika mji huu anatakiwa afanye pupa awe ni mwenye kujilazimisha kufuata amri za Allaah" mwenye kujilazimisha kumtii Allaah na kumtii Mtume wake ﷺ" na awe na tahadhari kubwa ya kuingia katika bid'ah (uzushi) na maasia, kwani mambo mema katika mji huu yana jambo kubwa, na bid'ah na maasia katika mji huu yanahatari kubwa, kwani mtu anaye muasi Allaah kwenye eneo tukufu dhambi zake ni kubwa kuliko anayemuasi nje ya hapo, na mambo mabaya huzidishwa na huwa makubwa kwa kufanywa katika eneo tukufu.

Ya Tatu: Na Muislamu katika mji huu ajitahidi kuwa na fungu kubwa la biashara ya akhera ambayo faida zake ni maradufu, na hayo ni kwa kuswali swala atakazoziweza katika msikiti wa Mtume ﷺ, ili apate malipo makubwa yaliyoahidiwa na Mtume ﷺ aliposema:

« صَلاَةٌ في مسجدي هَذَا خَيْرٌ مِنْ أَلْفِ صَلاَةٍ فِيمَا سِوَاهُ إِلاّ الْمَسْجِدَ الْحَرَامَ

«

"Swala moja katika msikiti wangu ni bora kuliko swala alfu moja katika misikiti mingine iispokuwa Masjidul Haram" [Amepokea Bukhari na Muslim].

Ya Nne: Ni kuwa: Muislamu katika mji huu wenye kubarikiwa ni kiigizo chema katika kheri. kwani yeye anaishi katika mji ambao "Nuru ilitoa mwangaza kutoka mji huo. na watu wenye kuongoza walio wema walitoka katika mji huo kwenda katika nchi mbali mbali. (Anatakiwa awe mwema) ili anayefika katika mji huu apate kiigizo chema kwa wakazi wake na asifiwe kwa sifa nzuri na tabia tukufu, kisha arudi kwenye mji wake akiwa ameathirika na amepata faida kwa aliyoyaona katika kheri, na kudumu katika kumtii Allaah na kumtii Mtume wake ﷺ.

na kama anavyopata faida mwenye kufika katika mji huu (faida za kheri na wema kwa kuona kiigizo kizuri katika mji huu uliobarikiwa); mambo yanakuwa kinyume iwapo ataona mtu aliye kinyume cha hivyo. kwa hiyo badala yakuwa ni mwenye kupata faida na mwenye kusifu, anakuwa ni mwenye kupata madhara na kukashifu.

Ya Tano: Muislamu akiwa Madina akumbuke kuwa : yuko katika ardhi nzuri ambayo ni mashukio ya wahyi na marejeo ya Imani na njia ya Mtume Mtukufu ﷺ na maswahaba wake watukufu ambao ni muhaajireen na Answar (waliopita juu ya ardhi hii kwa kheri na kwa kulazimiana na haki na uongofu). kwa hiyo atahadhari kukhalifu njia waliyopita maswahaba. kwa kuwa kukhalifu njia hiyo; ni kumuudhi Allaah (عز وجل) na pia kutawasababishia madhara na mwisho mbaya hapa duniani na kesho akhera.

Ya Sita: mtu ambaye Allaah amemuafikisha kuishi Madina ajihadhari kuzusha ndani yake uzushi au kumnusuru mzushi, kwani jambo hilo husababisha kupata laana. imethibiti kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema:

«الْمَدِينَةُ حَرَمٌ فَمَنْ أَحْدَثَ فِيهَا حَدَثًا أَوْ آوَى مُحْدِثًا فَعَلَيْهِ لَعْنَةُ اللّهِ وَالْمَلاَئِكَةِ وَالنّاسِ أَجْمَعِينَ لاَ يُقْبَلُ مِنْهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَدْلٌ وَلاَ صَرْفٌ »

"Mji wa Madina ni Mtukufu, mwenye kuzusha ndani yake uzushi au akamnusuru mzushi imshukie juu yake laana ya Allaah na Malaika na watu wote, haitakubaliwa kwake siku ya qiyama ibada ya faradhi wala ya Sunnah"

[Amepokea Muslim; kutoka katika hadeeth ya Abu Hureirah (رضي الله عنه) . na hadeeth hiyo iko katika sahihi mbili za bukhari na muslim katika hadeeth ya 'Ali (رضي الله عنه)]

Ya Saba: asikate miti au kuwinja kiwinjwa huko Madina. kwa makatazo yaliokuja katika jambo hilo katika hadeeth za Mtume ﷺ aliposema:

« إِنّ إِبْرَاهِيمَ حَرّمَ مَكّةَ وإِني حَرّمْتُ الْمَدِينَةَ مَا بَيْنَ لاَبَتَيْهَا لاَ يُقْطَعُ عِضَاهُهَا وَلاَ يُصَادُ صَيْدُهَا »

"Hakika Ibrahim ameiharamisha Makkah na mimi nimeiharamisha Madina: sehemu iliyo baina ya mitaa yake miwili, haikatwi miti yake, na hakiwindwi kiwindwa chake"

[Ameipokea Muslim kutoka kwa Jabir ibn 'Abdillaah].

Na amepokea tena Muslim katika hadeeth ya Saad ibn Abi Waqqaas (رضي الله عنه) kwamba Mtume ﷺ amesaema:

« إني أُحَرِّمُ مَا بَيْنَ لاَبَتَي الْمَدِينَةِ أَنْ يُقْطَعَ عِضَاهُهَا أَوْ يُقْتَلَ صَيْدُهَا »

"Mimi nimeharamisha sehemu zilizo baina ya mitaa miwili ya Madina kukatwa miti yake, au kuuwawa kiwinjwa chake."

Na katika sahihi mbili kutoka kwa 'Aasim ibn Suleiman Al-Ahwal alisema; "nilimwambia Anas: Jee Mtume ﷺ ameiharamisha Madina? Akasema ndio; sehemu iliyo baina kadha mpaka kadha haikatwi miti yake, mwenye kuzusha ndani yake uzushi imshukie laana ya Allaah na Malaika na watu wote"

Na katika sahihi mbili kutoka kwa Abu Hureirah (رضي الله عنه) kwamba: yeye alikuwa akiseama: “Lau ningeona paa huko Madina wanakula majani nisinge wafukuza.” amesema Mtume ﷺ:

« مَا بَيْنَ لاَبَتَيْهَا حَرَامٌ »

“Sehemu iliyoko baina ya mitaa yake mwili ni haramu (nitukufu)”

Na makusudio ya mti ulio haramishwa kukatwa ni ule ambao ulioteshwa na Allaah (عز وجل) . { yaani hawakuupanda viumbe}ama mti ambao ulipandwa na watu, yafaa kuukata.

Ya Nane: Ni Muislamu kusubiri dhiki ya maisha inayompata au balaa au shida yoyote. kwa maneno ya Mtume ﷺ katika hadeeth ya Abu Hureirah (رضي الله عنه) aliposema:

« لاَ يَصْبِرُ عَلَى لأْوَاءِ الْمَدِينَةِ وَشِدّتِهَا أَحَدٌ مِنْ أمتي إِلاّ كُنْتُ لَهُ شَفِيعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَوْ شَهِيدًا »

“Hakuna Muislamu yoyote katika umati wangu atakaesubiri shida za Madina ispokuwa nitakuwa mwenywe kumuombea shifaa siku ya qiyama au atakuwa shahidi” [Ameipokea Muslim]

Na pia katika swaheeh Muslim tunakuta kuwa: Abu Sa’eed Maula al-Mahri (aliyeachwa huru na huyu Mahri) alikuja kwa Abu Sa’eed al-Kudhree (رضي الله عنه) katika nyusiku za harra. Akanitaka shauri kutoka pale Madina na akamshtakia bei zake na wingi wa watoto wake, na akamweleza kuwa hawezi kusubiri dhiki ya Madina na shida zake. akamwambia “ole wako! Sikuamrishi hivyo nilimsikia mtume wa alla ﷺ akisema:

« لاَ يَصْبِرُ أَحَدٌ عَلَى لأْوَائِهَا فَيَمُوتَ إِلاّ كُنْتُ لَهُ شَفِيعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِذَا كَانَ مُسْلِمًا »

"Hakuna yoyote atakaye subiri shida za Madina kisha akafa ispokuwa nitakuwa mwenye kumwombea shifaa siku ya qiyama akiwa ni Muislamu."

Ya Tisa: Atahadhari kuwaudhi watu wa Madina. kwani kuwaudhi waislamu kila mahali ni haramu, lakini hilo katika mji Mtukufu ni haram zaidi. amepokea Bukhari katika swaheeh yake kutoka kwa Sa'ad Ibn Abee Waqqaas (رضي الله عنه) amesema: nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

« لاَ يَكِيدُ أَهْلَ الْمَدِينَةِ أَحَدٌ إِلاّ انْمَاعَ كَمَا يَنْمَاعُ الْمِلْحُ في الْمَاءِ »

"Hakuna yeyote atakaye wafanyia vitimbi watu wa Madina isipokuwa huyayuka kama chumvi inavyoyayuka katika maji"

Na amepokea Muslim katika swaheeh yake kutoka kwa Abu Hureirah (رضي الله عنه). amesema Mtume ﷺ:

« مَنْ أَرَادَ أَهْلَ هَذِهِ الْبَلْدَةِ بِسُوءٍ - يَعْنِى الْمَدِينَةَ - أَذَابَهُ اللّهُ كَمَا يَذُوبُ الْمِلْحُ في الْمَاءِ »

"Mwenye kutaka kuwafanyia ubaya watu wa mji huu- yaani Madina, Allaah humyayusha kama chumvi inavyoyayuka katika maji."

Ya Kumi: mkaazi wa Madina asighurike kuwa katika wakaazi wake kisha akasema, "Mimi ni katika wakazi wa Madina niko katika kheri!" Kwani kukaa pekee bila ya kuwa na 'matendo mema na kulazimiana na twa'a ya Allaah na Mtume wake ﷺ na kuwa mbali na madhambi na maasia hakumfaidishi kitu, bali madhara yatamrudia mwenyewe.

Na katika 'al-Muwatta' ya Imaam Maalik imekuja kwamba: Salmaan Al-Faarisee amesema: "Hakika nchi haimtukuzi mtu yoyote ispokuwa linalomtukuza mtu ni matendo yake", na sanadi yake ina kukatika ndani yake, lakini maana yake ni swaheeh. na hiyo ni habari yenye kuafikiana na ilivyo sawa; Amesema Allaah (عز وجل):

« إِنّ أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللّهِ أَتْقَاكُمْ »

"hakika Mtukufu wenu kwa Allaah ni yule mchaji Mungu wenu" [Hujurat – 49:13]

Na katika mambo yanayojulikana ni kwamba: katika zama mbali mbali mji wa madina una watu wema na watu waovu, hao watu wema matendo yao ndio yatakayo wanufaisha, na hao watu wabaya, Madina haiwezi ikawatukuza na kuinua jambo lao. na hilo ni kama nasaba, kwani mtu kuwa na nasaba nzuri tu bila ya matendo mema; hakuwezi kumnufaisha kwa Allaah. kwa maneno ya Mtume ﷺ: aliposema:

«وَمَنْ بَطّأَ بِهِ عَمَلُهُ لَمْ يُسْرِعْ بِهِ نَسَبُهُ »

"Na mtu ambaye matendo yake yamemchelewesha, nasaba yake haitamharakisha"

[Ameipokea Muslim katika swaheeh yake]

Kwa hiyo mtu ambaye matendo yake yamemchelewesha kuingia peponi nasaba yake haiwezi kumharakisha.

Ya Kumi na Moja: muislam awapo Madina ahisi kuwa yuko katika mji ambao nuru na elimu vimeenea ulimwengu mzima kutokea hapo, kwa hivyo afanye pupa kupata elimu ya kisheria ambayo itampeleka kwa Allaah kwa ujuzi [yaani itamuonyesha njia sahihi za kupita ili kufika kwa alla akiwa ameridhiwa] na atamlingania mtu mwengine kwa ujuzi, hasa hasa ikiwa kutafuta elimu ni

katika msikiti wa Mtume ﷺ. kwa hadeeth ya Abuu Hureirah (رضي الله عنه)

kwamba; alimsikia mtume wa alla ﷺ akisema:

« مَنْ دَخَلَ مَسْجِدَنَا هَذَا لِيَتَعَلّمَ خَيْراً أَوْ لِيُعَلِّمَهُ كَانَ كَالْمُجَاهِدِ فِي سَبِيلِ اللّهِ وَمَنْ دَخَلَهُ لِغَيْرِ ذَلِكَ كَانَ كَالنّاظِرِ إِلَى مَا لَيْسَ لَهُ »

"Mwenye kuingia katika msikiti wetu huu kwa ajili ya kujifundisha kheri au kuifundisha anakuwa kama mwenye kupigana jihadi katika njia ya Allaah, na mwenye kuingia msikitini kwa isiyokuwa hayo, anakuwa ni kama mwenye kuangalia mambo yasiomhusu."

[Amepokea Ahmad na ibn Maajah na wengineo, na hadeeth hiyo ina ushahidi wake katika at-Twabaraani katika hadeeth ya Sahli ibn Sa'ad (رضي الله عنه)]

Na kama ukaazi wa Madina una adabu, pia kuzuru Madina kuna adabu zake.

na mwenye kuzuru Madina anawajibika kuchunga adabu za ukaazi wa Madina zilizotangulia kwa ujumla, na inatakikana kujua kwamba linalotakiwa katika haki ya anaetaka kufika Madina, akusudie katika safari yake hiyo kuzuru msikiti wa Mtume ﷺ na kufunga safari kwa ajili ya msikiti huu. kwa maneno ya Mtume ﷺ yasemayo:

« لاَ تُشَدُّ الرِّحَالُ إِلاّ إِلَى ثَلاَثَةِ مَسَاجِدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ، وَمَسْجِدِ الرّسُولِ - صلى الله عليه وسلم - وَمَسْجِدِ الأَقْصَى »

"Haifungwi misafara isipokuwa kwenda katika misikiti mitatu: Masjid ul-Haraam, na msikiti wangu huu, na Masjid al-Aqswa" [Amepokea Bukhari na Muslim]

hadeeth hii inafahamisha kuzuiwa kufunga safari kwenda mahali popote - msikiti au kitu kingine - kwa ajili ya kujikurubisha kwa Allaah katika sehemu hiyo. kwa hadeeth iliyoko katika Sunan An-Nasaa'ee kutoka kwa Abuu

Hureirah (رضي الله عنه) amesema: “Nilikutana na Basra ibn Abi Basra Al-Ghifaari (رضي الله عنه) akaniuliza, ‘watoka wapi? Nikasema, ‘natoka Jabal at-Toor’, akasema: ‘lau ningekutana nawe kabla huja kwenda usingelikwenda.’ Nikamwambia: ‘kwa sabaabu gani?’ Akasema: ‘nilimsikia Mtume ﷺ akisema:

« لاَ تُعْمَلُ الْمَطِي إِلاّ إِلَى ثَلاَثَةِ مَسَاجِدَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ ومسجدي وَمَسْجِدِ بَيْتِ الْمَقْدِسِ »

“Haifungwi safari ispokuwa kwenda katika misikiti mitatu – yaani, Masjidul Haraam, na msikiti wangu na masjid Baitil Maqdis”

Na hiyo ni hadeeth swaheeh.

Na hadeeth hiyo ameitolea dalili Basra ibn Abi Basra al Ghifaari juu ya kuzuiwa kufunga safari kwenda katika misikiti au vitu vyengine isipokuwa misikiti hii mitatu.

Na mwenye kufika mji huu uliobarikiwa, anatakiwa azuru misikti miwili na makaburi matatu. Ama misikiti miwili ni msikiti wa Mtume ﷺ na msikiti wa Qubaa’, na zimepita baadhi ya dalili zinazo elezea fadhla za kuswali katika misikiti hiyo. ama makaburi matatu yanayotakiwa kuzuru ni kaburi la Mtume ﷺ na kaburi mbili za Maswahaba wake; Abubakar na “Umar (رضي الله عنهما) na makaburi ya Baqee na makaburi ya Mashahidi wa vita vya Uhud.

mwenye kuzuru kaburi la Mtume ﷺ na makaburi ya Maswahaba wake wawili (رضي الله عنهما) atakuja kwa upande wa mbele, kisha alielekee kaburi, na azuru ziyara ya kisheria. na atahadhari na ziyara ya uzushi.

Ziyara ya kisheria ni kumpa salamu Mtume ﷺ na kumuombea duwa kwa adabu na kwa sauti ya chini; atasema:

”Assalamu alyeka ya Rasoolullaah Warahmatullahi wabarakaa’tuh Sallallaahu wasallam wabaarak ‘alayka wajaazaka afdhwala maa jazaa nabiyyan ‘an ummatihy”.

Kisha atamtolea salamu Abubakar (رضي الله عنه) na atamuombea duwa, kisha atamtolea salamu "Umar (رضي الله عنه) na atamuombea duwa.

katika mambo ambayo yanatakiwa kujulikana ni kuwa: hawa watu wawili watukufu na makhalifa wawili waongofu wamekirimiwa na Allaah, na hawakukirimiwa wengine kama walivyo kirimiwa wao. Ama Abubakar (رضي الله عنه): Allaah alipomtuma Mtume wake ﷺ kwa haki na uongofu; yeye alikuwa wa kwanza kumuamini Mtume katika wanaume, na akawa pamoja nae huko Makkah baada ya kupewa Utume kwa muda wa miaka 13, na Allaah alipomruhusu Mtume wake kuhamia Madina, Abubakar alisuhubiana nae njiani, na Allaah akateremsha Qur'an inayosomwa kuhusu jambo hilo, nalo ni neno la Allaah (عز وجل):

« إِلّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنّ اللّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيّدَهُ بِجُنُودٍ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ »

"Ikiwa hamtomnusuru hakika alla amemnusuru pindi makafiri walipomtoa,{katika mji wa makka}. wakiwa wawili, wakati walipokuwa katika pango; pindi alipomwambia rafiki yake: "Usihuzunike, hapana shaka Allaah yupamoja nasi." Na Allaah aliteremsha utulivu wake juu yake na alimtilia nguvu kwa majeshi msioyaona. Na aliufanya ukafiri kuwa ni dhalili na Uislamu (ndio) wenye kushinda na Allaah ni mtukufu, Mwenye hikma."

Na akawa naye kule Madina kwa muda wa miaka kumi, na akahudhuria vita vyote pamoja naye. Na mtume ﷺ alipokufa, akatawala Ukhalifa baada yake na akasimamia vizuri jambo hilo. Na alipokufa Abubakar radhi za alla

zimuendee, Allaah akamkirimu kwa kuzikwa jirani na Mtume ﷺ na atakapofufuliwa atakuwa pamoja naye peponi. hizo ni fadhla za Allaah, anampa amtakaye, na Allaah ni mwenye fadhla kubwa.

ama "Umar ibn Khattab (رضي الله عنه) karibu watu arubaini walimtangulia kwenye Uislamu, na alikuwa ni mkali kwa Waislamu, Allaah alipomuongoza kwenye Uislamu nguvu zake na ukali wake ukawa kwa Makafiri, na Uislamu wake ukawa ni Utukufu kwa Waislamu. kama alivyosema 'Abdillaah ibn Mas'ood (رضي الله عنه) "Tuliendelea kuwa watukufu tangu aliposilimu 'Umar" [Ameipokea Bukhari katika swaheeh yake].

Na alikuwa pamoja na Mtume kule Makkah na akahama pamoja naye kuelekea Madina, na alihudhuria vita vyote pamoja naye. Na alipotawala Abubakar (رضي الله عنه) baada ya Mtume 'Umar alikuwa ni mkono wake wa kulia(msshauri wake na msaidizi wake mkubwa), kisha akatawala ukhalifa baada ya Abubakar, na akakaa katika ukhalifa zaidi ya miaka kumi.ikafunguliwa miji mingi katika ukhalifa wake na likapanuka eneo la miji ya kiisalmu na zikamalizwa dola mbili kubwa katika zama hizo. Dola la faaris na Dola la rum, na mali ya kisra na Qaisar ikatolewa *Fee sabeeli-llaah* kama alivyoilezea Mtume msema kweli mwenye kusadikishwa ﷺ.
Na hayo yalikuwa katika mikono ya 'Umar al-Faarooq (رضي الله عنه).

Na umar alipokufa ; Allaah akamkirimu kuzikwa jirani ya Mtume ﷺ, na atakapofufuliwa atakuwa pamoja naye peponi. na hiyo ni fadhla ya Allaah anampa amtakaye. na Allaah ni mwenye fadhla kubwa.

Hivi mfano wa hawa watu wawili wakubwa ambao hii ndio hali yao na hizi ndio fadhla zao; hivi inakubalika mtu awafanyie husuda au awatukane? *"Naudhubillahi minal khidhlaan."*

« رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلِإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالْإِيمَانِ وَلَا تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلًّا لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ »

[Hashir: 59:10]

"ewe mola wetu, tusamehe , na wasamehe pia ndugu zetu waliotutangulia katika imani, wala usitujaalie katika nyoyo zetu kuwa na donge dhidi ya waumini, ewe mola wetu hakika wewe ni mpole na mwenye kurehemu."

« رَبَّنَا لَا تُزِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ»

[Aali-'Imraan 3:8]

"Ewe mola wetu usizipindishe nyoyo zetu baada ya kutuongoza, na tupe rehma kutoka kwako , hakika wewe ni mwingi wa kutoa"

Na ibn katheer (رحمه الله) amenukuu katika tafsiri yake katika neno la Allaah (سبحانه وتعالى) lisemalo:

« إِنْ تَجْتَنِبُوا كَبَائِرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ نُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُمْ مُدْخَلًا كَرِيمًا»

"Mkijiepusha na madhambi makubwa mliyokatazwa tutawafutieni madhambi madogo na tutawaingizeni mahali patukufu peponi."[an-Nisaa 4:31]

Kutoka kwa ibn Abee Haatim kwa isnaad yake mpaka kwa Al-Mughira ibn Miqsam kwamba yeye amesema: "Ilikuwa ikisemwa: kumtukana Abubakar na 'Umar ni katika madhambi makubwa, 'Kisha akasema ibn Katheer: 'Nikasema:

na kundi la wanachuoni limesema kwamba: akufurishwe mwenye kuwatukana maswabaha", na haya ni mapokezi ya Maalik ibn Anas (رحمه الله).

Na Muhammad ibn Seerin amesema "Simdhanii yoyote kuwa anamchukia Abubakar na 'Umar na huku anampenda Mtume ﷺ. [Ameipokea at-Tirmidhee]

NA AMA ZIARA YA UZUSHI NI ILE INAYOKUSANYA MAMBO MENGI

La kwanza: Nikumuomba mtume ﷺ na kumtaka aokoe na kukidhi haja na kuondosha mateso, au mengineo katika mambo ambayo hayatakiwi ispokuwa kwa Allaah. kwani kuomba ni ibada na ibada, hafanyiwi ispokuwa Allaah peke yake, na Mtume ﷺ amesema:

« الدُّعَاءُ هُوَ الْعِبَادَةُ »

"dua ni ibada"

[na hiyo ni hadeeth swaheeh ameipokea Abu Daawud na Tirmidhi na wengineo]

Na amesema Tirmidhi: hii ni hadeeth Hasan swaheeh.

Na ibada ni haki ya Allaah. Na jambo lolote katika haki za Allaah haifai kumfanyia asiyekuwa Allaah, kwani hivyo ni kumshirikisha Allaah na kitu chengine. na Allaah Mtukufu ndiye anayetarajiwa ndiye anayeombwa. ama Mtume ﷺ huombewa na haombwi. na vile vile wengine katika waliokufa huombewa na hawaombwi, na katika mambo yanayojulikana ni kuwa; Mtume ﷺ yuko hai katika kaburi lake uhai wakibarzakhi uliokamili kuliko uhai wa mashahidi. na namna ya uhai huu haujui ispokuwa Allaah.

Na uhai huu unatofautiana na uhai kabla ya kufa na uhai baada ya kufufuliwa na kukusanywa. kwa hiyo haifai kumuomba Mtume ﷺ wala

kumtaka uokovu Kwani hiyo ni ibada na ibada hafanyiwi ispokuwa Allaah peke yake kama ilivyotangulia.

La pili: Kuweka mikono yake juu ya kifua chake kama namna ya swala. kwani hilo halifai; kwa sababu hiyo ni sifa ya unyenyekevu na kujidhalilisha kwa Allaah (عز وجل).

hiyo inatakiwa katika swala; wakati muisilamu akiwa kwenye swala akimuomba Mola wake. na maswhaba walivyokuwa na Mtume ﷺ katika uhai wake; walikuwa wanapofika kwake hawaweki mikono yao juu ya vifua vyao wanapompa salamu, na lau hilo lingekuwa ni kheri wangetutangulia kulifanya.

La tatu: kupangusa kuta na madirisha yalio kando kando ya kaburi la Mtume ﷺ na vile vile mahali popote katika msikiti au pahali pengine. kwani hilo halifai kwa sababu haikuja sunnah ya kufanya hivyo, na si katika vitendo vya watu wema waliopita. na hilo ni sababu ya ushirikina. na huenda anayefanya hivyo akasema : "mimi nafanya hivi kwa kumpenda Mtume ﷺ". Jawabu lake nikuwa: kumpenda Mtume ﷺ yapasa kuwe katika moyo wa kila Muislamu zaidi kuliko kuwapenda wazazi wake na watoto wake na watu wote, kama alivyosema ﷺ:

« لاَ يُؤْمِنُ أَحَدُكُمْ حَتّى أَكُونَ أَحَبّ إِلَيْهِ مِنْ وَالِدِهِ وَوَلَدِهِ وَالنّاسِ أَجْمَعِينَ

»

"*Hawi muumini mmoja wenu mpaka awe ananipenda zaidi kuliko wazazi wake na watoto wake na watu wote*" (ameipokea Bukahri na Muslim)

bali mapenzi ya Mtume yapasa kuwa ni zaidi kuliko mtu kuipenda nafsi yake. kama ilivyothibiti katika hadeeth ya 'Umar katika "saheehil Bukhari."isemayo: Na hakika yamepasa mapenzi ya Mtume ﷺ kuwa ni zaidi kuliko mapenzi ya nafsi, mzazi na mtoto. kwa sababu neema aliyoileta Allaah kwa waislamu imepitia katika mikono ya Mtume ﷺ. nayo ni neema ya uislamu; neema ya kuongozwa kwenye njia iliyonyooka, neema yakutolewa katika giza kupelekwa katika mwangaza, hiyo ni neema kubwa kulilko zote, hakuna neema inayolingana au kufanana nayo. Lakini kupangusa juu ya kuta za madirisha si alama ya kumpenda Mtume, bali alama yake nikumfuata Mtume ﷺ na kutekeleza sunnah zake, kwani dini ya kiislamu imejengwa kwa mambo mawili makubwa: la kwanza; nikutoabudiwa isipokuwa Allaah.

La pili; ni kutoabudiwa isipokuwa kwa kuafiki aliyokuja nayo Mtume ﷺ. na haya ndiyo madhumuni ya shahadatu allailaha illa LLAH na shahadatu Anna Muhammadu Rrasulullah. na kuna aya katika Quaran tukufu baadhi ya maulana wanaiita aya ya mtihani. nayo ni maneno ya Allaah (عز وجل) yasemayo:

« قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللّهَ فَاتّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَاللّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ »

[Aali-'Imraan 3:31]

Sema: mkiwa mnampenda Allaah nifuateni Allaah atakupendeni na atakusameheni madhambi yenu na Allaah ni mwingi wa kusamehe mwingi wa rehma.

Amesema Al- Hassan al-Basree na wengine katika salaf: kuna watu walidai kwamba wanampenda Allaah, Allaah akawapa mtihani kwa aya hii. na maana ya neno lao "*Ibtalahum*" aliwapa mtihani ili abainike mkweli na mrongo, kwani anaedai kumpenda Allaah na Mtume wake ﷺ anawajibika kuleta ushahidi juu ya madai yake, na ushahidi ni kumfuata Mtume ﷺ.

Amesema ibn katheer (رحمه الله) katika tafsiri ya aya hii: aya hii tukufu inamhukumu kila anaedai kumpenda Allaah na asiwe katika njia ya Muhammad, ni mrongo katika jambo hilo mpaka afuate sheria ya Muahmmad, na dini ya Mtume(katika maneno yote na vitendo vyote) kama ilivyothibiti katika hadeeth swaheeh kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema:

« مَنْ عَمِلَ عَمَلاً لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا ، فَهُوَ رَدٌّ »

"Mwenya kufanya tendo ambalo haliko katika dini yetu , tendo hilo ni lenye kurudishwa."

Na kwa hivyo amesema Allaah (عز وجل):

إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللّهَ فَاتّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللّهُ

"Mkiwa mnampenda Allaah basi nifuateni atakupendeni Allaah." [Aali-'Imraan 3:31]

Maana yake; mtapata zaidi ya mlivyotaka ambavyo ni kumpenda kwenu Allaah na yeye atakupendeni . na hili ni kubwa zaidi kuliko la kwanza kama walivyosema baadhi ya ma-'Ulamaa: yaani si jambo kubwa kupenda ispokuwa jambo kubwa ni kupendwa na alla. Kisha wakataja maneno yaliotangulia ya Al-Hassan al-Basree na wengineo katika maSalaf. Na amesema Imaan an-Nawawiy katika '*Majmoo' Sharh ul Muhadh-Dhab*' katika swala la kupangusa na kubusu ukuta wa kaburi la mtume ﷺ:" wala usidanganyike kwa kuona watu wengi wameenda kinyume, kwani kufuata na kutekeleza ni kwa kufuata hadeeth na maneno ya 'Ulamaa, na hayazingatiwi mambo yanayozushwa na watu kwa ujinga wao.

Na imethibiti katika '*sahihi mbili*' kutoka kwa "Aaisha (رضي الله عنهما) kwamba Mtume wa Allaah ﷺ amesema:

« مَنْ أَحدَثَ فِي دِينِنَا هَذَا مَا لَيسَ مِنهُ فَهُوَ رَدّ »

"Mwenye kuzusha katika dini yetu hiii lisilomo, jambo hilo atarejeshewa mwenyewe"

Na katiba mapokezi ya Muslim:

« مَنْ عَمِلَ عَمَلاً لَيْسَ عَلَيْهِ أَمْرُنَا ، فَهُوَ رَدٌّ »

"Mwenye kufanya 'jambo ambalo halipo katika dini yetu basi 'jambo hilo ni lenye kurejeshwa."

Na kutoka kwa Abu Hureirah (رضي الله عنه) amesema: Amesema mtume ﷺ:

« لَا تَجْعَلُوا قبري عِيدًا وَصَلُّوا عَلَي فَإِنّ صَلَاتَكُمْ تبلغني حَيْثُ كُنْتُمْ »

"Msifanye kaburi Langu kuwa ni 'Idd na niswalieni, kwani swala zenu zinanifikia kokote mlipo". [Ameipokea Abu Daawud kwa Isnaad iliyo swaheeh]

Na amesema al-Fudhail ibn 'Iyadh (رحمه الله) *"Fuata njia za uongofu na usikudhuru uchache wa wenye kufuata, na tahadhari na njia za upotevu na usikudanganye wingi wa wenye kuangamia."*

Na mwenye kupita katika akili yake kwamba; kupangusa kwa mkono na mfano wake kunazidisha Baraka, basi hilo ni katika ujinga wake na kupotea. Kwani Baraka hupatikana katika mambo yanayowafiki Sheria, na vipi hutakwa fadhla kwa kupinga njia sahihi?." Mwisho wa maneno ya imaam al nawawy (رحمه الله).

La Nne: Kufanya twawafu katika kaburi la Mtume, kwani hilo ni haramu. kwa sababu Allaah hakuweka twawaf ispokua kando kando ya Al-ka'bah Tukufu. Amesema Allaah (عز وجل):

« وَلْيَطَّوَّفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ »

"Na waizunguke Nyumba kale (Nyumba Kongwe – al-Ka'bah) [Al-Hajj 22:29]

Kwa hiyo hapafanyiwi twawaf mahali popote isipokua kando kando ya Al-Ka'bah Tukufu, na kwahivyo husemwa : watu wangapi wenye kuswali kwa ajili ya Allaah kila pahali. na vilevile husemwa: ni wangapi wanao toa sadaka kwa ajili ya Allaah, na wangapi wenye kumtaja Allaah. lakini hapasemwi: Ni wangapi wenye kutufu kwa ajili ya Allaah kila mahali? kwa sababu twawaf ni mambo yanayohusu Al-Ka'bah peke yake.

Amesema Sheikh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah (رحمه الله): "Na wameafikiana Waislamu kwamba haikuwekwa twawafu isipokua katika Al-Ka'bah, kwa hivyo haifai kufanya twawaf katika jiwe la Baitul-Maqdis wala katika chumba cha Mtume ﷺ wala katika Kubba lililoko katika Mlima wa 'Arafaat wala vitu vingine.

La Tano: Kuinua sauti mbele ya kaburi la Mtume ﷺ. kwasababu hilo halifai; kwani Allaah amewafundisha adabu Waumini walipokuwa na Mtume ﷺ akasema:

« يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آَمَنُوا لَا تَرْفَعُوا أَصْوَاتَكُمْ فَوْقَ صَوْتِ النَّبِيِّ وَلَا تَجْهَرُوا لَهُ بِالْقَوْلِ كَجَهْرِ بَعْضِكُمْ لِبَعْضٍ أَنْ تَحْبَطَ أَعْمَالُكُمْ وَأَنْتُمْ لَا تَشْعُرُونَ ۝ إِنَّ الَّذِينَ يَغُضُّونَ أَصْوَاتَهُمْ عِنْدَ رَسُولِ اللَّهِ أُولَئِكَ الَّذِينَ امْتَحَنَ اللَّهُ قُلُوبَهُمْ لِلتَّقْوَى لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ عَظِيمٌ »

"Enyi Mlioamini! Msipaze sauti zenu kuliko sauti ya Mtume, wala msiseme nae kwa sauti ya nguvu kama mnavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, vitendo vyenu visije vikakosa thawabu, na hali hamtambui. Kwa hakika wale wanaoangusha sauti zao mbele ya Mtume wa Allaah, hao ndio Allaah amezisafisha nyoyo zao kwa kumuogopa Allaah. Basi watapata Maghufira na thawabu kubwa (kabisa)." [Al-Hujuraat 49:2-3]

Na Mtume ﷺ ni mwenye kuheshimiwa katika uhai wake na baada ya kufa kwake.

La Sita: Kulielekea kaburi kutoka mahali palipo mbali na kumpa salamu Mtume ﷺ . sawa mtu alikuwa ndani ya msikiti au nje. amesema Sheikh wetu Sheikh ‘Abdul Aziz Ibn Baaz (رحمه الله) katika mansak yake “Na mtu huyo kwa ‘tendo hili yuko karibu zaidi na ugumu wa tabia yake, kuliko kupenda, na pia kuliko usafi wa tabia yake”.

Na katika mambo yanayotakiwa kuzindushwa ni kwamba: baadhi ya wanaofika Madina huwa wanausiwa na baadhi ya jamaa zao kufikisha salamu zao kwa Mtume ﷺ . na kwa kuwa haikuja hadeeth yoyote inayofahamisha hivyo, inatakikana kwa mwenye kuambiwa kufanya hivyo amwambie huyo anayemtuma kuwa: Kithirisha kumwombea rehema na amani Mtume ﷺ, na malaika watakufikishia kwa Mtume ﷺ. Na ushahidi wa hilo ni maneno ya mtume ﷺ: aliposema:

« إِنّ لِلّهِ مَلاَئِكَةً سياحين في الأَرْضِ يبلغوني مِنْ أمتي السّلاَمَ »

“*Hakika Allaah ana malaika wanaotembea katika ardhi, wananifikishia salamu kutoka kwa umati wangu*” [nayo ni hadeeth swaheeh ameipokea an-Nasa’ee na wengineo.]

Na kwa maneno ya Mtume ﷺ yasemayo:

« لاَ تَجْعَلُوا بُيُوتَكُمْ قُبُوراً وَلاَ تَجْعَلُوا قبري عِيداً وَصَلُّوا عَلَيّ فَإِنّ صَلاَتَكُمْ تبلغني حَيْثُ كُنْتُمْ »

“*Msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi na msilifanyie kaburi langu ‘Idd; na niswalieni kwani swala zenu zinanifikia popote mlipo*” [na hiyo ni hadeeth swaheeh ameipokea Abu Daawud na wengineo.]

Na katika mambo yanayotakiwa kujulikana ni kuwa: hakuna kulazimiana baina ya Hajj na 'Umrah na baina ya Ziara, kwa hiyo inawezekana kwa aliyekuja kuhiji au 'Umrah kurudi katika mji wake bila ya kwenda Madina, na aliyekuja Madina kutoka katika mji wake; anaweza akarudi bila kuhiji au kufanya 'Umrah, na anaweza akakusanya baina ya Hajj na 'Umrah na ziara katika safari moja.

Ama hadeeth zinazopokewa katika kuzuru kaburi la Mtume ﷺ mfano wa hadeeth isemayo "mwenye kuhiji na asinizuru basi amenichukia" na hadeeth "mwenye kunizuru baada ya kufa kwangu ni kama aliyenizuru katika uhai wangu" na hadeeth "Mwenye kunizuru na akamzuru baba yangu Ibrahim katika mwaka mmoja nitamdhaminia pepo kwa Allaah. Na hadeeth "mwenye kuzuru kaburi langu itamthibitikia shufaa yangu". [yaani maombezi yangu]

Hadeeth hizi zote na mfano wake hazina hoja yoyote, kwani hadeeth hizo ni maudhui au ni dhaif sana, kama walivyolieleza hilo waliohifadhi hadeeth, kama Ad-Daaraqutnee' na Al-'Uqaily na al-Baihaqee na Ibn Taymiyyah na Ibn Hajar (رحمهم الله).

Na ama maneno ya Allaah (عز وجل): yasemayo:

« وَلَوْ أَنّهُمْ إِذْ ظَلَمُوا أَنْفُسَهُمْ جَاءُوكَ فَاسْتَغْفَرُوا اللّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرّسُولُ لَوَجَدُوا اللّهَ تَوّابًا رَحِيمًا »

"Na lau wangalikuja walipojidhulumu nafsi zao (kwa kwenda kuhukumiwa na njia isiyokuwa ya Sheriya) wakaomba msamaha kwa Allaah, na Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Allaah ni Mwenye kupokea toba (na) Mwenye kurehemu."[An-Nisaa' 4:64]

Aya hiyo haina dalili yoyote ya kukusudiwa kaburi wakati mtu akiidhulumu nafsi yake na kutaka msamaha kwa Mtume ﷺ. kwani aya inaelezea wanafiki. Na kumjia Mtume ﷺ ilikuwa ni katika uhai wake: Kwani Maswahaba (رضي الله عنهم وأرضاهم) walikuwa hawaji katika kaburi lake kwa ajili ya kutaka maghfira, na ndio maana 'Umar ibn al-Khattab (رضي الله عنه) alitawasali kwa duwa ya Al-Abbass ulipowapata ukame, na akasema: *"Ewe mola wangu wa haki hakika sisi tulipokuwa tunapata ukame hutawasali kwako kupitia kwa Mtume wetu kisha wewe hutunyeshea mvua, na sasa tunatawasali kwako kupitia kwa 'Ammi wa Mtume wetu, basi tunyesheleze. Akasema: wakanyeshelezewa."* [ameipokea Bukhari katika swaheeh yake].

Iau ingekuwa kutawasali kwa Mtume ﷺ baada ya kufa kwake kunafaa 'Umar (رضي الله عنه) asingetawasali kwa al-'Abbass (رضي الله عنه).

Na pia dalili nyengine ya hayo ni hadeeth aliyoipokea Bukhari katika swaheeh yake katika; '*Kitabul-mardhwa*' kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنهما) kwamba amesema: "Ewe kichwa changu! mtume ﷺ akasema: "Iau kipindi hicho ningekuwa hai nikakutakia maghfira na kukuombea duwa" Akasema 'Aaisha "Ewe hasara yangu! Naapa kwa Allaah mimi nadhania kuwa wewe unapenda kufa kwangu… ".Iau mtume (صلى الله عليه وسلم) angekuwa ni mwenye kuombea duwa na msamaha baada ya kufa kwake, isingekuwepo tofauti kati ya kufa bibi 'Aaisha kabla ya Mtume au kufa Mtume kabla ya bibi 'Aaisha.

Na kuzuru kaburi la Mtume ﷺ: kumethibiti kwa hadeeth nyingi zenye kuthibitisha kuzuru makaburi, kama mtume ﷺ alivyosema:

« زُوروا القبور،فَإنّها تُذَكِّرُكُم الآخِرَةَ »

"Zuruni makaburi kwasababu yanakukumbusheni akhera" [amepokea Muslim katika swaheeh yake].

Lakini haitakikani kusimama sana mbele ya kaburi la Mtume ﷺ wala kukithirisha ziara, kwa sababu kufanya hivyo husababisha kupetuka mpaka. na Allaah (سبحانه وتعالى) Amemjaalia Mtume ﷺ (kinyume na watu wengine katika ummati wake) : kwamba malaika wanamfikishia salamu kutoka kila mahali. kwa qauli ya mtume ﷺ isemayo: *"hakika Allaah ana malaika wanaotembea katika ardhi wananifikishia salamu kutoka kwa umati wangu."* Na kwa maneno yake Mtume ﷺ *"msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi wala msilifanye kaburi langu kuwa ni 'Idd na niswalieni kwani swala zenu zinanifikia popote mlipo".*

na Mtume ﷺ alipokataza kufanywa kaburi lake kuwa 'Idd akaeleza jambo ambalo litakuwa badala yake kwa kusema kuwa *"Niswalieni kwani swala zenu zinanifikia popote mlipo"* anakusudia kuwa : anafikishiwa na Malaika.
ama kuzuru makaburi ya Baqee na kuzuru makaburi ya mashahidi wa uhud; hiyo ni Sunnah; itakapokuwa kwa njia ya kisheria. na itakuwa haramu itakapokuwa kwa njia ya uzushi. na ziara ya kisheria ni ile inayofanywa kwa kuafiq aliyokuja nayo Mtume ﷺ. Ziara inayo kusanya manufaa ya aliye hai (mwenye kuzuru) na manufaa ya maiti (mwenye kuzuriwa).

Kwani Mwenye Kuzuru Anapata Faida Tatu:

Faida ya kwanza kukumbuka mauti na kuyaandalia matendo mema. kwa maneno ya Mtume ﷺ aliposema: "Zuruni makaburi, kwa sababu yanakukumbusheni akhera" amepokea Muslim.

Na Faida ya pili ni huko kufanya ziara, kwani ziara ni Sunnah aliyoiweka Mtume ﷺ. kwa hiyo mtu hulipwa thawabu kwa ziara hiyo.

Na faida ya tatu ni kuwafanyia wema maiti wa kiislamu kwa kuwaombea duwa. na mtu atalipwa thawabu kwa wema huo.

ama maiti mwenye kuzuriwa: yeye anapata faida katika ziara ya kisheria, kwa kuombewa duwa na kufanyiwa ihsani, kwani maiti wanapata faida kwa duwa za walio hai.

Na ni Sunnah kwa mwenye kuzuru makaburi kuwaombea duwa maiti. kwa hadeeth zilizothibiti kutoka kwa Mtume ﷺ katika suala hilo. Na katika hizo, hadeeth ya Bureydah ibnul Huswaib (رضي الله عنه) amesema: "mtume ﷺ alikua akiwafundisha (duwa) wanapokwenda makaburini, akawa mtu anasema:

« السّلاَمُ عَلَيْكُمْ أَهْلَ الدّيَارِ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُسْلِمِينَ وَإِنّا إِنْ شَاءَ اللّهُ بكم لَلاَحِقُونَ أَسْأَلُ اللّهَ لَنَا وَلَكُمُ الْعَافِيَةَ »

"*Amani iwashukie enyi watu wa miji hii waumini na waislamu, hakika sisi ni wenye kukutana nanyi akitaka Allaah. Tunamuomba Allaah - atuondoshee tunayo yachukia.*" [Amepokea hadeeth hiyo Muslim]

Na kuzuru makaburi ni Sunnah kwa wanaume. ama kuzuru makaburi kwa wanawake: wanaachuoni wametofautiana katika hilo, kuna wanaojuzisha na kuna wanaokataa. Na qauli iliodhahiri katika kauli hizo mbili ni kutofaa. kwa maneno ya Mtume ﷺ: alipsema:

« لَعَنَ اللهُ زَوّارَاتِ الْقُبُورِ »

"*Allaah amewalaani wanawake wenye kuzuru makaburi*" [Ameipokea hadeeth hiyo Tirmidhi na wengineo. na akasema Tirmidhi: hiyo ni hadeeth Hasan swaheeh]

kwani maana iliyo wazi zaidi katika tamshi la "zawarati" ni *nisbah*. yaani kuinasibisha ziara kwa wanawake au wanawake wenye kufanya ziara. mfano wake ni kauli ya alla(عز وجل): isemayo:

« وَمَا رَبُّكَ بِظَلّامٍ لِلْعَبِيدِ »

"mola wako hakuwa ni mwenye kuwadhulumu waja." [Fussilat 41:46]

Yaani hakuwa mwenye kudhulumu au mwenye kunasibishiwa dhulma. na si maana yake kutia mkazo katika ziara, kama walivyosema baadhi ya wenye kujuzisha kuzuru makaburi kwa wanawake. pia kwa sababu ya udhaifu waliokuwa nao wanawake, na uchache wa subra, kwa kulia na kuomboleza.na vile vile qauli ya kuwazuia inaondoa shaka zaidi, kwani mwanamke akiacha kuzuru hatakosa isipokua jambo la Sunnah. na ikipatikana ziara kwake hujisababishia laana.

ama ziara ya uzushi (Bid'ah) ni ile inayofanywa kwa isiyokuwa njia ya kisheria; kama kukusudiwa makaburi kwa ajili ya kuwaomba maiti, na kuwataka waokoe watu, na kuwataka wakidhi haja zao, na mfano wa hayo. kwani maiti hapati faida na ziara hii, na kwa alie hai hupata madhara, kwasababu ya kufanya jambo lisilo faa. kwani huko ni kumshirikisha Allaah, na maiti hapati manufaa yoyote, kwani hakuombewa isipokuwa ameombwa yeye badala ya Allaah.

Na amesema Sheikh wetu, Sheikh Abdul Aziz Bin Baaz (رحمه الله) katika 'Mansak' yake: "Ama kuwazuru maiti kwa ajili ya kukusudia kuwaomba katika makaburi yao, au kukaa hapo, au kuwaomba wakidhi haja za watu, au wapoze wagonjwa, au kumuomba Allaah kupitia kwao, au kwa cheo chao; ziara hii ni uzushi ulio katazwa. hakuiweka Allaah wala Mtume wake, wala hawakuifanya watu wema waliopita (رضي الله عنهم).

bali ziara hiyo ni katika maneno mabaya aliyoyakataza Mtume ﷺ wakati aliposema: '*Zuruni makaburi na msiseme maneno mabaya*',

na mambo haya yaliotajwa hukusanyika kuwa ni bid'ah – Uzushi. lakini daraja zake zinatofautiana; baadhi yake ni uzushi na si ushirikina; (kama kumuomba Allaah (سبحانه وتعالى) katika makaburi kwa haki ya maiti na cheo chake. na mfano wa hayo). na baadhi ni katika ushirikina mkubwa; kama kuwaomba maiti na kuwataka msaada na mfano wa hayo.

Haya ndiyo niliyokusudia kuyataja. na namuomba Allaah (عز وجل) atuwafiqishe sisi, wenye kuishi Madina , wenye kuizuru Madina pamoja na waislamu wote, kufanya mambo ambayo husifiwa mwisho wake hapa ulimwenguni na akhera.na Aturuzuku maisha mazuri katika mji huu na adabu nzuri, na atupe mwisho mwema.

وصلى الله وسلم وبارك على عبده ورسوله نبينا محمد وعلى آله وأصحابه أجمعين

Tarehe 03.06.2010 sawa na 22 JAMADUL AKHAR 1431 A.H.